

HOTUBA YA MGENI RASMI MKUU WA
MKOA WA IRINGA MHE.AMINA MASENZA
KWENYE SHEREHE ZA MEIMOSI , 2017

- Katibu Tawala Mkoa,
- Katibu wa CCM Mkoa
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,
- Wah. Wenyeviti wa Halmashauri
- Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,
- Viongozi wa Dini,
- Mwenyekiti wa TUCTA Mkoa wa Iringa,
- Kamati ya Ulinzi na Usalama (M),
- Ndugu Makatibu Tawala Wilaya,
- Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri,
- Ndugu Wenyeviti na Makatibu wa Vyama huru vyaWafanyakazi,
- Ndugu Waajiri,
- Ndugu Wafanyakazi wote,
- Waandishi wa Habari,
- Wageni Waalikwa,
- Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote namshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa na afya njema.

Aidha, nawashukuru waandaaji kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani ambayo Kimkoa inafanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa. Kipekee, nawapongeza na kuwashukuru Viongozi wote wa Vyama huru vya wafanyakazi kwa kuratibu na kufanikisha zoezi zima la maandalizi.

Vile vile, nawapongeza wajumbe wa kamati mbalimbali za maandalizi, vikundi vya burudani pamoja na wafanyakazi na wananchi walioshiriki kwa hali na mali katika kufanikisha maadhimisho haya na kuyafanya

yafane. Shughuli ni watu na inahitaji maandalizi.

Ndugu Wafanyakazi, Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana;

Kama mnavyofahamu Mei Mosi ni Siku ya Wafanyakazi Duniani kote. Katika kuadhimisha siku hii, Wafanyakazi hujumuika pamoja kwa lengo la kuwasilisha madai yao kwa waajiri, kupongezana kwa kufanya kazi vizuri, kushauriana kutekeleza majukumu kwa uaadilifu.

Ndugu Wafanyakazi, Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana;

Maadhimisho ya mwaka huu yamebeba kauli mbiu isemayo“ UCHUMI WA VIWANDA

UZINGATIE HAKI, MASLAHI NA HESHIMA YA WAFANYAKAZI "

Kaulimbiu hii, tunapaswa kuitekeleza kwa vitendo kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria zilizopo. Kila mmoja wetu anapaswa kutimiza wajibu wake, sote kwa pamoja tukifanya hivyo tutaondoa malalamiko yasiyo ya lazima mahali pa kazi na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Ndugu Wafanyakazi, Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana;

Serikali inatambua mchango wa wafanyakazi wa kada zote waliopo serikali na waliopo katika taasisi binafsi, yapo mambo mengi mliyoyafanya yenye manufaa kwa Taifa letu na Mkoa wetu kwa ujumla, mumeendelea kutoa huduma mbalimbali katika jamii mfano

mumeboresha huduma za afya, upatikanaji wa maji safi na salama

Pia kwa kupitia utumishi wenu uliotukuka Mkoa wetu umeendelea kufanya vizuri katika zoezi la uandikishaji wa vyeti vya kuzaliwa vyeti vya uraia, kuongezeka kwa ufaulu wa watoto shule za msingi na sekondari.

Aidha, itakumbukwa miaka ya nyuma kulikuwepo na kero nyingi zilizokuwa zikiwakabiri wafanyakazi, kama vile ucheleweshaji wa mishahara, malipo kwa wastaafu. Kwa kutambua hayo Serikali imeendelea kuzifanyia kazi kero hizo mwaka hadi mwaka na sasa hali inazidi kuimarika ingawa maboresho hayajafikia kiwango cha asilimia mia moja.

vilevile, Serikali inatambua kwamba zipo Kero kubwa zinazowakabili watumishi hususani mishahara midogo nakuwepo kwa kodi kubwa ambayo haiendani na hali halisi ya kiuchumi. Katika kurekebisha haya Serikali imeendelea kutafutia ufumbuzi wa kudumu ambapo kuanzia mwaka 2016 Serikali ilifanya marekebisho makato ya kodi ya mishahara ya 11 % na kufikia 9 %. Tunaimani kuwa Serikali itaendelea kufanya marekebisho zaidi pale itakapobidi.

Vilevile nawaagiza waajiri wote wenye madeni sugu ya watumishi yakiwemo ya matibabu, masomo ,uhamisho,nauli za likizo na madai mengine ambayo ni stahiki za wafanyakazi kuyalipa mara moja pia wahakikishe na kuhakikisha hawasababishi madeni mengine mapya.

Aidha kuhusu wafanyakazi kuwa na makazi bora kama vile ambavyo watu wengine wanaishi kwenye makazi bora tutaendelea kulishauri shirika la nyumba (NHC) kujenga nyumba zenye gharama nafuu ambazo watumishi wataweza kumudu kununua ,pia nishauri kwamba watumishi hakikisheni fedha mnazozipata mnazitumia kwenye mambo ya msingi ikiwa ni pamoja kujiunga kwenye vikundi mbalimbali vya kiuchumi na SACCOS ili muweze kujiinua kiuchumi badala ya kutegemea mishahara pekee.

Ndugu Wafanyakazi;

Mtambue kwamba Kila kazi ina taratibu zake, tunapodai mabadiliko lazima tuzingatie taratibu zilizopo haki ni lazima iendane na kutimiza wajibu. Lazima tufanye kazi,

tuipende na kuiheshimu kazi na tuwajibike ipasavyo. Tutambue kuwa Maadili ya kazi kwa kila Mtumishi ni ya msingi sana. Ili mfanyakazi yeyote aweze kuheshimika inampasa kuelewa umuhimu wa nafasi yake katika jamii anayoihudumia, kwa kufanya kazi kwa juhudi, weledi, nidhamu na kwa malengo. tuisubiri kusukumwa sukumwa katika kutekeleza majukumu yetu.

Ndugu Waajiri,

Waajiri mnawajibu mkubwa wa kuhakikisha kazi zinafanywa kwa ufanisi, mshikamano na uadilifu. Jukumu la kutoa vitendea kazi bora kwa watumishi ni lenu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mtumishi anakuwa na mazingira bora, safi na salama yanayomuwezesha kufanya kazi pasipo kuwa na tatizo lolote. Pia wapeni motisha wafanyakazi wenu pale

wanapofanya vizuri na pale wanapofanya vibaya hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao, kwani Uhai wa taasisi yoyote ile unategemea sana uwepo wa watumishi na hivyo tambueni umuhimu wao

Risala yenu Wafanyakazi wa Mkoa wa Iringa ,imezungumzia kuwa wapo baadhi ya waajiri ambao hawataki kufuata sheria kwa mfano kutounda Mabaraza ya Wafanyakazi, na yale yaliyoundwa kutokaa kwa mujibu wa Sheria nawaagiza waajiri wote ambao hamjaunda mabaraza ya wafanyakazi mhakikishe mnaunda na kwa yale mabaraza ambayo yameundwa lakini hayafanyi kazi hakikisheni yanakaa na kujadili mambo yanayowahusu watumishi ili wajue na kuwa na taarifa sahihi.

Kama mlivyoomba mngependa baadhi ya Viongozi wa vyama vya wafanyakazi waweze kuwakilisha katika vikao vya Kamati ya ushauri ya Mkoa (RCC), napenda nitamke kuwa tumelichukua na tutalifanyia kazi.

Vyama vya wafanyakazi,
Vyama vya Wafanyakazi vinawajibu Mkubwa kuhakikisha ustawi wa wafanyakazi wao na waajiri unakuwepo. Vyama vinatakiwa kuhakikisha watumishi wanapata elimu zinazohusiana na masuala mbalimbali ili waweze kuendana na sayansi na teknolojia ya sasa na pia kuwasaidia wafanyakazi kutambua nafasi walizopewa katika jamii na kuelewa msingi wa utumishi bora kwa Umma. Vyama vya wafanyakazi kamwe visiwe ndio chanzo cha vurugu mahala pa kazi na

visifuge uzembe na ubadhilifu wowote unaofanywa unaofanywa mahali pakazi.

Ndugu Wafanyakazi, Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana;

Pamoja na maelezo niliyoyatoa, kumekuwepo na changamoto mbalimbali kwa baadhi ya wafanyakazi, kama vile: -

- Baadhi ya Wafanyakazi kutokuwa waadilifu kulikosababisha kuwepo na watumishi hewa na watoro.
- Baadhi ya Wafanyakazi kutotunza siri za serikali na Taasisi wanakofanyia kazi kumesababisha nyaraka kufika mikononi mwa watu wasiostahili.
- Baadhi ya Wafanyakazi wanalalamikiwa kwa vitendo vya rushwa hasa katika utoaji wa huduma mbalimbali.

- Baadhi ya Watumishi kuwa chanzo cha kuchochea migogoro mahala pa kazi.

Mapungufu haya yote lazima yafanyiwe kazi kwa kuzingatia taratibu zilizopo na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika.

Wafanyakazi, Wageni waalikwa Mabibi na Mabwana;

Napenda pia kukumbusha janga la UKIMWI, ambalo limeendelea hupunguza nguvu kazi kila mahala. Tuendeleo kukumbushana kwamba hakuna dawa ya UKIMWI ila kubadili tabia.

Muhimu ni kwamba waliokwisha pata maambukizi, naomba wafuate ushauri wa Madaktari. Kwa wale ambao hawajapata VVU/Ukimwi wawe makini, Serikali itaendelea

kutoa dawa za kupunguza makali, ili maisha yaendeleee.

Ndugu wafanyakazi,

Lishe ni suala mtambuka na ni agenda kuu ya Mkoa ni lazima akina mama na akina baba nilazima tuhakikishe tunalisha familia zetu chakula bora. Tafiti zinaonyesha Kiasi cha udumavu na ukondefu kwa watoto wadogo ni kikubwa na mkoa wetu ni miongoni mwa Mikoa yenye udumavu wa watoto pamoja na kwamba tunachakula cha kutosha, hivyo tushirikiane sote kutoa elimu ya lishe ili jamii na hasa watoto na akina mama wajawazito wote tuwapatie chakula bora ili wawe na afya njema.

Ndugu Wafanyakazi,

Sote ni walezi wa familia, hususani sisi wafanyakazi tuna changamoto kubwa kuwa muda mwingi tunaututumia katika ajira zetu na kusahau majukumu yetu ya msingi ya ulinzi na usalama wa watoto wetu hivyo niwaombe kwa pamoja kutimiza wajibu wa kuhakikisha watoto wanakuwa salama, kukemea vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia hususani ubakaji na ulawiti ambao umeendelea kujitokeza. Unyanyasaji huu, kibaya zaidi umekuwa ukiwahusisha watu wazima na watoto wadogo. Hivyo daima tuhakikishe usalama wao kwa kuwajibika kikamilifu katika kuwalinda na kuwahakikishia ustawi wa maisha yao.

Pia ndugu Watumishi tuendeleo kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Iringa kuhakikisha tunatunza mazingira kwa ujumla.

Mwisho,

Nawashukuru washiriki wote walioshiriki maadhimisho haya. Nawapongeza

wafanyakazi bora wote wa mwaka 2017.

Ufanyakazi bora wenu uwe chachu na hamasa kwa wafanyakazi wenzenu.

Waajiri muendeleee kuboresha thamani ya zawadi mtoazo ili iwe kichocheo cha uzalishaji wenye tija. Baada ya kusema haya machache, Naahidi kero zilizopo ndani ya uwezo wa Mkoa zitafanyiwa kazi na zile za kitaifa zitapelekwa ngazi za juu ili ziweze kutafutiwa ufumbuzi.

Ninawatakia kila la kheri katika utendaji kazi kwenye maeneo yenu.

Asanteni